JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 08 - 2020/2021**

**DHIDI YA**

**RADIO FREE AFRICA**

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kurusha Matangazo (Matangazo ya Redio) kwa Kituo cha **Radio Free Africa** kwa ajili ya kutoa huduma ya utangazaji wa maudhui kwa njia ya redio.

1.2 Tarehe 29 Julai, 2020 kati ya Saa 12.00 na Saa 12.30 asubuhi, Kituo cha **Radio Free Africa** kinatuhumiwa kukiuka Kanuni na Maadili ya Utangazaji kupitia kipindi cha ***Amka na BBC*** kwa kurusha maudhui bila kuzingatia mizania ya habari pale walipokuwa wakimhoji Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Bw. Tundu Lissu juu ya viongozi wa chama hicho kutoshiriki katika kutoa heshima za mwisho kwa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa.

1.3 Mtangazji wa kipindi hicho wakati akimhoji Bw. Tundu Lissu aliruhusu kurushwa kwa habari iliyoegemea upande mmoja pale Bw. Tundu Lissu alipotoa tuhuma na kulalamika kuwa Serikali ilimnyima nafasi ya kutoa heshima za mwisho kwa Hayati Benjamin William Mkapa, bila kumtafuta Msemaji wa Serikali ili aweze kutolea ufafanuzi tuhuma hizo, jambo ambalo ni kinyume na Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji wa Habari.

1.4 Wakati wa kipindi cha ***Amka na BBC***, Bw. Tindu Lissu alisikika akizungumza maneno yafuatayo:

***"...Inasikitisha sana, tumefika kwa wakati tulioambiwa kwa mujibu wa ratiba. Kutuambia kwamba hatuwezi kuingia uwanjani kwa sababu tumechelewa tuliona ilikua ni namna tu ya kusema kwamba hawataki tushiriki kumuaga huyu aliyekuwa Rais wetu...Haiwezekani tena kama hutakiwi na waandaaji wa msiba ukilazimisha kwenda watakwambia wewe ndo mchawi. Sisi hatutaki kuonekana ni wachawi wa mzee Mkapa tumesema waendelee tu Mungu awabariki.".***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kitendo cha **Radio Free Africa** kurusha kipindi kilichoituhumu Serikali bila ya kuthibitisha ukweli wa madai yaliyotolewa katika taarifa hiyo kutoka kwenye vyanzo husika na kutozingatia mizania, **Radio Free Africa** wanatuhumiwa kukiuka Kanuni Na.15(2) (b) na (c) na Na. 16 za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018; ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

*15. (2) The licensee shall-*
*(b) report accurately, impartially, fairly and in a non- partisan manner;*
*(c) report news in an objective and balanced manner, without intentional or negligent departure from the facts, whether by distortion, exaggeration, misrepresentation or material omission.*

*16. A content service licensee shall ensure that, during the presentation of current affairs programme, factual programmes and documentaries; where issues of public importance are discussed, reasonable effort is made and reasonable opportunity is given to present a fair, accurate, balanced and impartial view.*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI

Tarehe 05 Agosti, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Radio Free Africa,** wito wa kuwasilisha utetezi wao wa maandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kujieleza dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

Tarehe 10 Agosti, 2020, Uongozi wa **Radio Free Africa** uliwasilisha utetezi wa maandishi uliosainiwa na **Samwel Nyalla**, Mkurugenzi wa **Radio Free Africa.** Pia, tarehe hiyo hiyo, Uongozi huo ukiwakilishwa na **Samwel Nyalla**, **Abdul Diallo**, Mkurugenzi wa Vipindi, **Benedict Ishabakaki**, Mshauri wa Sheria, **Neriah Martin**, Mwanasheria, **Michael Noel**, Mtangazaji na **Joan John** ulifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 KUSOMEWA SHITAKA NA KUSIKILIZA MAUDHUI YA RADIO FREE AFRICA

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **Radio Free Africa** shitaka lao. Pia, Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Radio Free Africa** walisikiliza maudhui yaliyochapishwa na kutangazwa na **Radio Free Africa** katika

tarehe tajwa hapo juu na kisha kuualika Uongozi huo kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni au la.

## 5.0 UTETEZI WA RADIO FREE AFRICA

Katika maelezo yao ya maandishi, **Radio Free Africa** walikiri kurusha kipindi kinachotuhumiwa kukiuka Sheria na Kanuni na walisema wanatambua kuwa kwa mujibu wa Kanuni za Maudhui, kila chombo cha habari kinatakiwa kuhakikisha taarifa zote zinazorushwa zinakidhi vigezo ikiwemo mizania ya pande zote zilizohusishwa katika taarifa hiyo.

Walisema kuwa taarifa inayotuhumiwa na iliyorushwa katika kipindi cha **Amka na BBC** ilikuwa ni muendelezo wa taarifa za **BBC** zilizorushwa kupitia **Radio Free Africa** kuanzia tarehe 28 Julai, 2020 katika kipindi cha **Dira ya Dunia (Saa 12:30 hadi Saa 1:30 jioni)** na zilizohusu msiba wa Hayati Benjamin William Mkapa. Walidai kuwa taarifa hii inayotuhumiwa, ya tarehe 29 Julai, 2020 ilikuwa ni muendelezo wa taarifa ya tarehe 28 Juilai, 2020 ambapo **BBC** ilitamka hewani kuwa ilifanya jitihada za kumtafuta Msemaji wa Serikali lakini hazikufanikiwa na kwamba walikuwa wanaendelea na jitihada za kupata msimamo wa Serikali kuhusu suala hilo.

Walimaliza kwa kueleza kuwa washirika wao, **BBC** ambao ndiyo wazalishaji wa kipindi cha **Amka na BBC** kinachorushwa na **Radio Free Africa**, walifanya kila linalowezekana kuweka mizania katika habari hiyo ingawa jitihada hizo hazikufanikiwa, hivyo waliisihi Kamati isichukue hatua za kisheria dhidi yao.

Pia, **Radio Free Africa** ilitoa utetezi wao wa mdomo kama ifuatavyo:

4.1 **Samwel Nyalla** alikazia utetezi wao wa maandishi na kuikabidhi Kamati "flash disk" iliyokuwa na rekodi ya vipindi vya **BBC** vilivyorushwa na **Radio Free Africa**, tarehe 28 Julai, 2020 na 29 Julai, 2020. Pia, aliikabidhi Kamati nakala za barua pepe walizowasiliana na **BBC Swahili** kuhusu wito wa Kamati ambapo **BBC** waliwajibu kuwa wangewarudia ndani ya muda mfupi.

Wakati wa kujumuisha utetezi wao na baada ya kupokea maswali na hoja mbali mbali zilizotolewa na Kamati, **Samwel Nyalla** alisema kuwa wanauchukua ushauri mzuri wa Kamati kwamba wana wajibu wa kupokea kwa umakini mkubwa maudhui ya vyombo vya nje ya nchi kwa kuzingatia Uzalendo na Sheria za nchi.

Alimaliza kwa kuomba msamaha na kusema kuwa wanao uwezo wa kuwabana washirika wao, **BBC**, kuhusu maudhui yasiyofaa na mara kadhaa wameshawahi kusitisha kurusha maudhui yao yenye utata.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Radio Free Africa** imetenda kosa la kutangaza maudhui bila ya kuzingatia mizania ya habari kwa kushindwa kufanya juhudi zo zote za kutoa fursa kwa Serikali ili kutolea ufafanuzi tuhuma walizoruhusu zitangazwe kupitia chombo chao;

6.2 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba utetezi wa **Radio Free Africa** kuwa wazalishaji wa maudhui yanayotuhumiwa ni **BBC** hauna mashiko yo yote kwa sababu **Radio Free Africa** ndio wanamiliki leseni ya Utangazaji wa Habari hapa nchini, hivyo **Radio Free Africa** wana wajibu wa kuhakikisha kuwa maudhui yote wanayotangaza, yaliyozalishwa hapa nchini au wanayopokea kutoka vyombo vya habari vya nje ya nchi, yanazingatia Sheria, Kanuni, na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari, masharti ya leseni yao pamoja na Maadili na Utamaduni wa Mtanzania;

6.3 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa **Radio Free Africa** kuwa **BBC** walifanya jitihada za kumtafuta Msemaji wa Serikali lakini hazikufanikiwa hauna mashiko kwa sababu wao, **Radio Free Africa** waliotangaza habari ile kupitia chombo chao ndiyo walitakiwa kutafuta maoni ya upande wa Serikali;

6.4 Kamati ya Maudhui imeona kuwa hoja ya **Radio Free Africa** kuwa taarifa inayotuhumiwa ilikuwa ni muendelezo wa taarifa ya tarehe 28 Julai, 2020 haina msingi wo wote kwa sababu katika taarifa zote mbili, kila taarifa ilikuwa inajitegemea na hivyo walitakiwa kuzingatia matakwa ya kisheria ya kuzingatia mizania katika taarifa yao ya tarehe 29 Julia, 2020 inayotuhumiwa;

6.5 Kamati ya Maudhui imebaini kuwa **Radio Free Africa** wana Usimamizi dhaifu wa vipindi vyao hasa wanavyopokea na kuvirusha kutoka vyombo vya habari vya nje ya nchi, jambo lililosababisha kutangaza habari isiyokidhi matakwa ya kisheria na kisha wakashindwa kufanya jitihada zo zote za kumtafuta Msemaji wa Serikali;

6.6 Hivyo, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Radio Free Africa** imetenda kosa la kurusha kipindi kilichoituhumu Serikali bila ya kuthibitisha ukweli wa madai yaliyotolewa katika taarifa hiyo kutoka kwenye vyanzo husika na kutozingatia mizania ya Uandishi na Utangazaji wa Habari, kinyume na Kanuni Na. 15(2) (b) na (c) na Na. 16 za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

## 7.0 USHAURI WA KAMATI KWA RADIO FREE AFRICA

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Radio Free Africa** kuimarisha Usimamizi wa maudhui yao ili kuepuka utangazaji wa maudhui yanayovunja Sheria, Kanuni, Weledi na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari;

Pia, **Radio Free Africa** wanashauriwa kupitia upya mikataba yao na vyombo ya utangazaji wa habari vya nje ya nchi ili kuhakikisha masharti ya mikataba yao yanazingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari pamoja na masharti ya leseni yao.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kuutafakari kwa kina utetezi uliotolewa na Uongozi wa **Radio Free Africa**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **Radio Free Africa** wamekiuka Kanuni tajwa za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

Hivyo basi, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **Radio Free Africa:**

1. Wanapewa Onyo Kali;

2. Wanawekwa chini ya uangalizi kwa muda wa miezi mitatu (3) pamoja na kutahadharishwa kuwa hatua kali zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi yao iwapo hawatajirekebisha na kurudia makosa kama hayo ndani ya muda tajwa.

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **14 Agosti, 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Joseph Method Mapunda**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S.L.P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

..............................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Abdul Ramadhani Ngarawa**......................................

2. **Derek Kaitira Murusuri**......................................

3. **Jacob Gregory Tesha**......................................